OFISI YA WAZIRI MKUU

SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU



Rais wa Jamhuri ya Namibia, Mhe. Dkt. Netumbo Nandi-Ndaitwah leo, ametembelea kiwanja cha Ubalozi wa Namibia kilichopo katika Mji wa Serikali Mtumba, Jijini Dodoma.

Akiwasili katika Mji huo, Mhe. Rais Dkt. Netumbo Nandi-Ndaitwah alipokelewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi.

Mhe. Rais Dkt. Netumbo Nandi-Ndaitwah



# MATUKIO KATIKA PICHA

## BUNGENI

Kikao cha 58 cha Bunge la 13 Mkutano wa 3









# Wakandarasi Watakiwa Kukamilisha Miradi Kwa Wakati

## Mji Wa Serikali, Mtumba



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Prof. Palamagamba Kabudi, amesema Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kuwekeza katika maendeleo ya Mji wa Serikali, Mtumba, ili kuimarisha utoaji wa huduma za Serikali na kuongeza ufanisi wa utendaji wa taasisi za umma. Amesisitiza kuwa utekelezaji wa azma hiyo unategemea pia wakandarasi kukamilisha miradi wanayopewa kwa wakati na kwa kuzingatia viwango vya ubora vinavyotakiwa.

Prof. Kabudi amesema hayo leo, tarehe 19 Juni, 2026, alipokagua maendeleo ya ujenzi wa Mji wa Serikali, Mtumba, jijini Dodoma. Alieleza kuridhishwa na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika ujenzi wa majengo ya Wizara, taasisi na miundombinu muhimu.



Amesema uwekezaji mkubwa uliofanyika jijini Dodoma, hususan katika Mji wa Serikali, unaakisi dhamira ya Serikali ya kuimarisha makao makuu ya nchi kwa viwango vya kimataifa. Kutokana na mafanikio hayo, Prof. Kabudi amesema kuna kila sababu ya kumpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na uamuzi wa kuendelea kuwekeza katika maendeleo ya Mji wa Serikali.

Tanzania Yaeleza Mafanikio ya Ujumuishwaji wa Watu Wenye Ulemavu, Yaahidi Kuimarisha Upatikanaji wa Teknolojia Saidizi.



Serikali ya Tanzania imeeleza mafanikio makubwa iliyoyapata katika kuimarisha ustawi na ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu, huku ikisisitiza umuhimu wa kuongeza upatikanaji wa vifaa na teknolojia saidizi ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Akihitimisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 19 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (COSP19-CRPD) uliofanyika New York, Marekani, Juni 11, 2026, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi, amesema teknolojia na vifaa saidizi vina mchango mkubwa katika kuwawezesha watu wenye ulemavu kuishi kwa kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii.

“Ni muhimu kuendelea kuongeza upatikanaji na matumizi ya vifaa na teknolojia saidizi kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi kwa usawa pia Serikali inaendelea kutekeleza kwa vitendo dhana ya ujumuishwaji kwa kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata fursa na haki kwa usawa katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi,” alisema Mhe. Mahundi.



Akizungumza kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. James Kilabuko, amesema ushiriki wa Tanzania katika mkutano huo umeiwezesha nchi kujifunza uzoefu na mbinu mbalimbali za kukabiliana na changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu.



“Tanzania imepiga hatua kubwa katika uwezeshaji na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu hivyo Kupitia mkutano huu, tumejifunza mbinu na uzoefu kutoka mataifa mbalimbali ambazo zitatusaidia kuimarisha zaidi juhudi zetu, lakini pia Serikali itaandaa mpango kazi mahususi kwa kushirikiana na wizara, taasisi na wadau mbalimbali ili kuendeleza utekelezaji wa masuala ya watu wenye ulemavu na kushughulikia changamoto zilizobainishwa wakati wa mkutano huu.,” alisema Dkt. Kilabuko.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Serikali, Dkt. Grace Maghembe, amesema Tanzania imeendelea kuboresha huduma za afya za msingi kwa watu wenye ulemavu kwa kusogeza huduma karibu na wananchi kuanzia ngazi ya jamii, sambamba na kuboresha miundombinu ya afya na kuwajengea uwezo watumishi wa sekta hiyo katika utoaji wa huduma jumuishi.

# OWM, DIT yaingia makubaliano kuimarisha usimamizi wa maafa nchini



SERIKALI kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) imeingia Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) yenye lengo la kuimarisha usimamizi wa maafa nchini kwa kutumia sayansi, teknolojia na ubunifu.

Akizungumza mapema hii leo katika hafla ya utiaji saini wa makubaliano hayo Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Dkt. Jim Yonazi, amesema hatua hiyo ni utekelezaji wa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kujenga mifumo madhubuti ya kiutendaji inayoongozwa na maarifa, sayansi na teknolojia ikiwemo matumizi ya Akili Unde (AI) katika kukabiliana na maafa.

Dkt. Jim Yonazi



Amesema makubaliano hayo yanatekeleza pia mapendekezo ya Mkutano wa Nane wa Umoja wa Mataifa wa Jukwaa la Dunia la Upunguzaji wa Vihatarishi vya Maafa uliofanyika Geneva, Uswisi, mwezi Juni 2025, na yanaashiria mabadiliko ya kimkakati katika namna Serikali inavyoshughulikia changamoto za maafa kutoka mfumo wa kusubiri majanga hadi mfumo wa kujikita katika kinga, maandalizi na tahadhari.

Dkt. Jim Yonazi
Katibu Mkuu

# OWM yasisitiza ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu katika mipango ya taifa



SERIKALI imeendelea kusisitiza dhamira yake ya kuhakikisha Watu Wenye Ulemavu wanapata nafasi sawa katika nyanja zote za maendeleo, ikiwa ni pamoja na kijamii, kiuchumi na kisiasa, kupitia sera, sheria na mipango jumuishi inayotekelezwa nchini.

Hayo yamebainishwa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) Dkt. Jim Yonazi wakati wa ufunguzi wa kikao kazi kilichowakutanisha viongozi wa vyama vya Watu Wenye Ulemavu na mashirika yasiyo ya kiserikali kujadili utekelezaji wa sera, sheria na miongozo ya ujumuishaji nchini

Amesema hatua kubwa zimeendelea kuchukuliwa katika kuhakikisha hakuna mwananchi anayeachwa nyuma, ambapo Sera ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 pamoja na Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 zimekuwa msingi muhimu wa utekelezaji wa haki na usawa kwa kundi hilo.






“Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa kila sera, mpango na huduma inayotekelezwa nchini inazingatia ujumuishaji wa Watu Wenye Ulemavu tangu hatua ya upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji hadi tathmini, ili kuhakikisha hakuna anayebaki nyuma,” amesema Dkt. Jim Yonazi.



# Serikali yasisitiza umuhimu wa uadilifu katika utumishi wa umma



SERIKALI imeendelea kusisitiza umuhimu wa kuzingatia misingi ya uadilifu katika utumishi wa umma ili kuhakikisha utekelezaji wa majukumu na mipango ya maendeleo unafanyika kwa ufanisi na kwa kuzingatia maadili ya kazi.

Hayo yamesemwa hii leo  na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Dkt. Jim Yonazi, wakati akifungua Mafunzo ya Kamati ya Uadilifu yaliyolenga kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati Maalum ya Menejimenti katika kusimamia masuala ya uadilifu katika ofisi hiyo.





"Uadilifu ni nguzo muhimu katika ufanikishaji wa majukumu na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika sehemu za kazi," amesema Dkt. Yonazi.

Dkt. Jim Yonazi
Katibu Mkuu



## Serikali yazitaka taasisi zote kujiandaa kukabiliana na athari za el niño.

SERIKALI imesema itaendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa maafa nchini ili kupunguza madhara yanayosababishwa na majanga mbalimbali ambayo yamekuwa yakigharimu maisha ya watu, kuharibu mali na kurudisha nyuma maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
Kauli hiyo imetolewa hii leo na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Dkt. James Kilabuko, wakati akifunga Jukwaa la Wadau wa Usimamizi wa Maafa lililojadili Rasimu ya Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kuzuia na Kukabiliana na Madhara ya El Niño Jijini Dodoma.

Amesema Tanzania imeendelea kukabiliwa na matukio ya maafa yanayosababisha athari kubwa kwa wananchi na uchumi wa Taifa, hali inayolazimu kuwepo kwa maandalizi madhubuti ya kukabiliana na changamoto hizo kabla hazijatokea.

"Nchi yetu imekuwa ikishuhudia matukio ya majanga ambayo yamekuwa yakisababisha maafa na kuathiri mfumo wa kawaida wa maisha ya jamii. Majanga hayo yamesababisha vifo, ulemavu wa kudumu, upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu," amesema Dkt. Kilabuko.

# JARIDA LA MTANDAONI
# OFISI YA WAZIRI MKUU
# SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU




Ofisi Ya Waziri Mkuu

Mji wa Serikali, Mtumba, 40412
S.L.P 980, Dodoma Tanzania.

ps@pmo.go.tz

+255262322480

Nukushi: +255262324534.


